



## KONGAMANO LA ISHIRINI NA TANO LA KISWAHILI Bayreuth, tarehe 18 hadi tarehe 20 mwezi wa tano 2012

Tarehe 20, mwezi wa  
Januari, 2012

Wapendwa mabibi na mabwana!

Tuna furaha kubwa kuwaalika kongamano la ishirini na tano litakayofanyika hapa Ujerumani katika Chuo Kikuu cha Bayreuth.

Kongamano letu la Kiswahili limeshaota mizizi hapa katika Chuo Kikuu cha Bayreuth. Kila mwaka linawakaribisha watalamu wa masomo mbalimbali wanaofanya uchunguzi kuhusu vipengele kadha vya Kiswahili (ama Viswahili) na tamaduni zao. Upana wa mada zinazohusu Kiswahili na huzungumziwa kwenye Kongamano, kama vile isimu ya Kiswahili, fasihi ya Kiswahili, mada za anthropolojia kuhusu Kiswahili na utamaduni wake historia ya lugha hii na fasihi yake. Watalamu kutoka pembe mbalimbali za dunia na masomo tofauti hubadilishana mawazo. Pia sisi huwakaribisha washabiki na wasanii wa fani mbalimbali za Kiswahili. Mbali na kuwakaribisha wale ambao wamezoea kuja Bayreuth, tunafurahi kuwakaribisha watalamu na wanafunzi wapya kwetu pia. Kawa kawaida huwa tunakutana kwenye mkahawa siku moja kabla ya kongamano. Mara hii tutakutana Alhamisi tarehe 17 Mei 2012. Jina la mkahawa na saa ya kukutana tutataja baadaye.

### **Mada maalum**

Kongamano letu la Kiswahili kwa mwaka huu limefikia miaka 25, na kwa hivyo linastahiki kutazamwa kwa jicho la sherehe ya *jublei* – kwa hivyo, kwanza tungelipenda kuadhimisha siku hii ya kufikia miaka 25 ya Kongamano la Kiswahili kwa kupendekeza mada kuu itayoshughulikia suala la umri wa kongamano lenyewe. Yaani kufikia kwake miaka 25. Pili, kwa sababu mnamo miaka hii 25, dhana tatu muhimu zimejitokeza kwa nguvu kubwa katika matumizi ya chambuzi mbalimbali za taaluma. Hizi ni dhana za *utandawazi* (globalisation), dhana ya *baadaye-(ya)-ukoloni* (postcoloniality/ postcolonialism) na dhana ya *usasabaadaye* (postmodernism). Dhana hizi zitumike katika uchambuzi wa Kiswahili, isimu yake, fasihi yake, utamaduni wake na historia yake. Pia, kwa kawaida, tunawapa wanakongamano nafasi ya kuandika juu ya mada yoyote ile itayohusiana na Kiswahili na vipengele vyake vyote kwa mtazamo wowote usiohusika na dhana hizo tatu zilizotajwa hapo juu.

### **Kujiandikisha**

Tunakaribisha mada zenu katika lugha ya Kiswahili ama Kiingereza. Kila uwasilishaji wa mada pamoja na majadiliano unakadiriwa kuchukua muda wa dakika thelathini tu.

Tafadhalini, mjiandikishe kutoa makala, pia mjiandikishe hata ikiwa hamtatoa makala, kwa njia ya baruapepe (**swahili@uni-bayreuth.de**) mpaka kufikia tarehe **30 Machi 2012**. Iwapo mtatoa makala yenu kwa Kiswahili, tafadhalini muandike pia muhtasari mfupi kwa Kiingereza.

### **Pahala/ wakati**

Pahala pa Kongamano hili patakuwa Iwalewa-Haus, Münzgasse 9. Kongamano litaanza siku ya Ijumaa tarehe 18, mwezi wa tano, saa tatu asubuhi na litamalizika Jumapili tarehe 20. Kumalizika kwa kongamano kutategemea idadi ya mawasilisho tutakayopewa.

Muda si mrefu utaweza kupata barua hii, ratiba na habari mpya kwenye ukurasa wa mtandao ufuatao:

[http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili\\_colloq1/index.html](http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq1/index.html)

### **Malazi**

Kwenye ukurasa wa mtandao mtapata habari za malazi. Iko orodha ya hoteli pia (maelezo hayo yanatokana na Idara ya Utalii ya mji wa Bayreuth). Suala la malazi na chakula mtajitegemea. Lakini baadhi ya wanafunzi wetu watawakaribisha wanafunzi kutoka vyuo vikuu vyingine wakae nyumbani mwao kwa muda wa kongamano. Wanafunzi wanaotaka kupata malazi kwa wanafunzi wetu, watuarifu mapema kwa njia ya baruapepe (tazama anwani yetu chini). Wanafunzi (chini ya umri wa miaka 25) wanaweza kupata malazi katika “Bweni la Vijana” (tazama: <http://www.jugendherberge.de/jh/bayern/bayreuth/>).

Barua ya pili ya mwaliko itakayoambatanishwa na mpangilio wa makala na utaratibu mzima wa semina itatumwa mwisho wa mwezi wa nne (Aprili).

Ikiwa mna maswali, msisite kutuandikia. Kwa mawasiliano zaidi, tumieni anwani yetu ya email: **swahili@uni-bayreuth.de**.

Tukiwa na matumaini ya kuonana katika Kongamano hili la 25 la Kiswahili hapa Bayreuth - twasema “Karibuni Sana.”

Prof. Said A. M. Khamis

Literaturen in afrikanischen Sprachen  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553598  
Fax.: +49-921-553641

Prof. Gabriele Sommer, Dr. Clarissa Vierke

Afrikanistik I  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553556  
Fax.: +49-921-553627